هدية
HADIYAH

# Uislamu

## Ni dini ya maumbile na akili na furaha

الإسلام دين الفطرة والعقل والسعادة

Kiswahili

سواحيلي


Kamati ya Kielimu ya usimamizi wa mambo ya Dini ya Msikiti Mtukufu wa Makkah na Madinah

# الإِسْلَامُ

# دِينُ الفِطْرَةِ وَالعَقْلِ وَالسَّعَادَةِ

**Uislamu**

**Ni dini ya maumbile na akili na furaha**

اللَّجْنَةُ العِلْمِيَّةُ

بِرِئَاسَةِ الشُّؤُونِ الدِّينِيَّةِ بِالمَسْجِدِ الحَرَامِ وَالمَسْجِدِ النَّبَوِيِّ

**Kamati ya Kielimu ya usimamizi wa mambo ya Dini ya Msikiti Mtukufu wa Makkah na Madinah**

بِسْمِ اللهِ الرَّحمَنِ الرَّحِيمِ

# Uislamu

## Ni dini ya maumbile na akili na furaha

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

Je, umewahi kujiuliza:

Ni nani aliyeumba mbingu na ardhi na vyote vilivyomo miongoni mwa viumbe vikubwa? Na ni nani aliyetengeneza mfumo huu nyeti wenye ufanisi mkubwa ndani yake?

Ulimwengu huu mkubwa umepangwaje na kuwa thabiti pamoja na mifumo yake inayoudhibiti kwa ustadi kwa miaka mingi?

Je, ulimwengu huu ulijiumba wenyewe? Au ulizuka pasina kutokea mahali? Au umepatikana ghafla?

### Nani aliyekuumba?

Ni nani aliyeweka mfumo huu nyeti kabisa katika vifaa vya mwili wako na katika miili ya viumbe hai wengine?

Hakuna anayeweza kukubali kuwa nyumba hii ilikuja pasina kujengwa na yeyote! Au mtu akamwambia kuwa kutokuwepo ndiko kuliko ileta nyumba hii! Ikiwa nyumba unayoishi hukubaliani na

hayo inakuwaje baadhi ya watu wanamuamini mwenye kuwaambia kuwa ulimwengu huu ulikuja wenye pasina muumbaji? Hivi anakubali vipi mwenye akili kuwa mpangilio huu wa ulimwengu wa hali ya juu ulitokea ghafla (kama mlipuko)?

Kwa msisitizo kabisa nikuwa kuna Mola Mtukufu muumbaji na mpangiliaji wa ulimwengu huu na vyote vilivyomo, naye ni Mwenyezi Mungu Aliyetakasika na kutukuka.

Na Mola Mlezi Aliyetukuka alitutumia mitume amani iwe juu yao, na akateremsha vitabu juu yao vya kiuungu (Wahyi), na kitabu cha mwisho ni Qur'ani alichokiteremsha Mwenyezi Mungu kwa Muhammadi wa mwisho katika mitume wa Mwenyezi Mungu, na kupitia vitabu vyake na mitume wake:

* Ametutambulisha yeye mwenyewe na sifa zake na haki zake juu yetu, na akatubainishia haki zake juu yetu.

* Na akatuelekeza kuwa yeye ndiye Mola Mlezi aliyeumba viumbe wote, nakuwa yeye yuko hai wala hafi, na viumbe wote wapo mikononi mwake na chini ya mamlaka yake na maamuzi yake.

Na akatueleza kuwa miongoni mwa sifa zake ni elimu, bila shaka amekizunguka kila kitu kwa elimu, nakuwa yeye ni msikivu mwenye kuona hakuna chochote kinachofichikana kwake ardhini wala

mbinguni.

Na Mola Mlezi ndiye aliye hai msimamizi wa mambo yote ambaye uhai wa kila kitu unatoka kwake pekee Aliyetakasika, na kuwa yeye ndiye msimamizi ambaye yanasimama maisha ya kila kiumbe kupitia yeye Mtukufu, amesema Mtukufu:

﴿اللَّهُ لا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ لا تَأْخُذُهُ سِنَةٌ وَلا نَوْمٌ لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الأَرْضِ مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلا يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِنْ عِلْمِهِ إِلَّا بِمَا شَاءَ وَسِعَ كُرْسِيُّهُ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضَ وَلا يَئُودُهُ حِفْظُهُمَا وَهُوَ الْعَلِيُّ الْعَظِيمُ ﴿٢٥٥﴾﴾

***"Mwenyezi Mungu - hapana mungu ila Yeye Aliye hai, Msimamia mambo yote milele. Hashikwi na usingizi wala kulala. Ni vyake pekee vyote vilivyomo mbinguni na duniani. Ni nani huyo awezaye kufanya uombezi mbele yake isipokuwa kwa idhini yake? Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao, wala wao hawajui vyema chochote katika vilivyo katika elimu yake, ila kwa atakalo mwenyewe. kiti chake kimeenea mbinguni na ardhini; na wala kuvilinda hivyo hakumshindi. Na Yeye ndiye aliye juu mno, Mkuu".***

[Suratul Baqara: 255].

* Na akatueleza kuwa yeye ndiye Mola Mlezi anayesifika kwa sifa kamilifu, na akaturuzuku akili na

hisia zinazoweza kufahamu maajabu ya uumbaji wake na uweza wake, jambo linalotuonyesha utukufu wake na nguvu zake na ukamilifu wa sifa zake, na akapandikiza kwetu sisi umbile linalotuonyesha juu ya ukamilifu wake nakuwa yeye haiwezekani asifike kwa upungufu.

* Na kujua kwetu kuwa Mola Mlezi yuko juu ya mbingu zake haimaanishi kuwa yuko ndani ya ulimwengu wala ulimwengu hauko ndani yake.

* Na akatueleza kuwa ni wajibu kwetu kujisalimisha kwake Mtukufu kwani yeye ndiye muumba wetu na muumba wa ulimwengu na mpangiliaji wake.

Hivyo muumba anasifa za utukufu na wala haiwezekani kamwe asifike nakuwa na hitajio au mapungufu, Mola Mlezi hasahau wala halali wala hali chakula, na wala haiwezekani kuwa na mke au mtoto; na kila andiko ambalo linapingana na utukufu wa muumbaji hilo si katika ufunuo sahihi waliokuja nao mitume wa Mwenyezi Mungu amani iwe juu yao.

Amesema Allah aliye takasika ndani ya Qurani Tukufu:

﴿قُلْ هُوَ ٱللَّهُ أَحَدٌ ۝١ ٱللَّهُ ٱلصَّمَدُ ۝٢ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ۝٣ وَلَمْ يَكُن لَّهُۥ كُفُوًا أَحَدٌۢ ۝٤﴾

***"Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni wa pekee****

***Mwenyezi Mungu ndiye Mkusudiwa ****

***Hakuzaa wala hakuzaliwa ****

***Wala hana anayefanana naye hata mmoja."***

[Al-Ikhlaas: 1-4].

Ukiwa unamuamini Mola Mlezi Muumbaji.... Hivi uliwahi kujiuliza hata siku moja kuhusu lengo la kuumbwa kwako? Na ni nini anakitaka Mwenyezi Mungu kwetu sisi, na lipi lengo la uwepo wetu sisi?

**Na je, inawezekana kuwa Mwenyezi Mungu alituumba kisha akatuacha hivhivi? Na je, inawezekana kuwa Mwenyezi Mungu aliumba viumbe vyote hivi pasina kuwa na lengo wala dhumuni yoyote?**

Uhalisia nikuwa Mola Mlezi Muumbaji Mtukufu (Allah) alitueleza kuhusu dhumuni la yeye kutuumba sisi, nalo ni kumuabudu Mwenyezi Mungu pekee, na ni nini anachotaka kutoka kwetu! na akatueleza kuwa yeye pekee ndiye anayestahiki kuabudiwa, na akatubainishia kupitia mitume wake amani iwe juu yake ni namna gani tutamuabudu? Na ni namna gani tutajiweka karibu kwake kwa kufanya maamrisho yake na kuacha makatazo yake? na ni namna gani tutapata radhi zake? na kuhadhari adhabu yake, na akatueleza kuhusu mafikio yetu baada ya kufa?

Na akatueleza kuwa maisha haya ya dunia si lolote

bali mtihani tu, nakuwa maisha ya kweli na ya uhakika na yaliyokamilika zaidi yatakuwa Akhera baada ya kufa.

Na akatueleza kuwa atakayemuabudu Mwenyezi Mungu kama alivyomuamrisha, na akayaacha aliyomkataza; basi atapata maisha mazuri duniani, na neema za kudumu Akhera, na atakayemuasi na akamkufuru basi atapata maisha ya shida katika dunia, na adhabu ya kudumu Akhera.

**Na kwakuwa tunajua fika kuwa sisi hatuwezi kuendesha maisha haya ya dunia pasina ya kila mtu kupata malipo ya yale aliyoyafanya kuanzia ya kheri au ya shari; kwa hivyo hapatokuwa na adhabu kwa madhalimu wala kuwalipa watenda wema?**

Na alitueleza Mola wetu Mlezi kuwa kufuzu kwa kuzipata radhi zake na kuokoka na adhabu yake hakuwi ila kwa kujisalimisha kwake na kumuabudu yeye pekee asiye na mshirika, na kunyenyekea kwa utiifu, na kutekeleza sheria zake kwa moyo mkunjufu na kukubali, na alitueleza kuwa yeye hakubali kutoka kwa watu dini isiyokuwa hiyo, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَمَن يَبْتَغِ غَيْرَ ٱلْإِسْلَٰمِ دِينًا فَلَن يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي ٱلْءَاخِرَةِ مِنَ ٱلْخَٰسِرِينَ ٨٥﴾

***"Na Mwenye kutafuta dini isiyokuwa dini ya Kiislamu, basi hiyo haitakubaliwa kwake, na yeye Akhera atakuwa ni miongoni mwa wenye kupata hasara".***

[Al-Imran: 85].

Mwenye kutazama vile wanavyoviabudu watu wengi leo hii; atakuta huyu anaabudu mtu, na mwingine anaabudu sanamu, na mwingine anaabudu nyota na kadhalika, na haifai kwa mwanadam mwenye akili timamu aabudu chochote isipokuwa Mola Mlezi wa walimwengu mkamilifu katika sifa zake, inakuwaje anaabudu kiumbe au chini ya kiumbe! Muabudiwa hawezi kuwa kiumbe au sanamu au mti au mnyama!

Dini zote wanazozitumia watu kuabudu leo hii -ukiacha Uislamu- Mwenyezi Mungu hazikubali kwani ni dini zilizotengenezwa na binadam, au dini ambazo zilikuwa ni za Mwenyezi Mungu kabla kisha zikachezewa na mikono ya mwanadam, ama Uislamu hiyo ni dini ya Mola Mlezi wa walimwengu, haitofautiani wala haibadiliki, na kitabu cha dini hii ni Qur'ani Tukufu, ni kitabu kilichohifadhiwa kama alivyokiteremsha Mwenyezi Mungu na bado kipo mikononi mwa waislamu mpaka leo hii tena kwa lugha yake kilichoteremshwa kwayo kwa Mtume wa mwisho.

Na miongoni mwa misingi ya Uislamu ni kuwaamini Mitume wote aliowatuma Mwenyezi Mungu, na wote walikuwa ni binadamu aliowatia nguvu Mwenyezi Mungu kwa alama na miujiza mbali mbali, na akawatuma kufikisha ujumbe wa kumuabudu yeye pekee asiye na mshirika wake,

Na wa mwisho katika Mitume ni Mtume Muhammadi rehema na amani ziwe juu yake, Mwenyezi Mungu alimtuma kwa sheria za mwisho za kiungu zilizokuja kufuta sheria za Mitume waliokuwa kabla yake, na akamtia nguvu kwa miujiza mikubwa, na kubwa zaidi ni Qur'ani Tukufu, maneno ya Mola Mlezi wa walimwengu, kitabu chake kitukufu zaidi wanadamu kuwa kukijua, ni muujiza katika madhumuni yake na lafudhi zake na mpangilio wake, na hukumu zake, ndani yake kuna muongozo wa kuipata haki unaompeleka mtu katika furaha duniani na Akhera, na kilitaremka kwa lugha ya kiarabu.

Na kuna ushahidi mwingi wa kiakili na wa kielimu (kisayansi) ambao unathibitisha pasina shaka yoyote kuwa Qur'ani hii ni maneno ya muumba Aliyetakasika na kutukuka nakuwa haiwezekani kuwa imetengenezwa na mwanadam.

Na miongoni mwa misingi ya Uislamu ni kuamini Malaika, na kuamini siku ya mwisho pale Mwenyezi Mungu atakapowafufua watu kutoka makaburini mwao siku ya Kiyama ili awahesabu kwa matendo yao,

atakayetenda mema hali yakuwa ni muumini basi atapa neema za kudumu peponi, na atakayekufuru na akatenda maovu basi atapata adhabu kubwa motoni, na miongoni mwa misingi ya Uislamu ni kuamini yale aliyoyapanga Mwenyezi Mungu katika mambo ya kheri au shari.

Na dini ya Uislamu ni mtaala ulioyaenea maisha yote, inaafikiana na maumbile na akili, na nafsi zilizo sawa zinaikubali, ameiweka kuwa sheria Muumba Mtukufu kwa ajili ya viumbe wake, na ndio dini ya kheri na furaha kwa watu wote katika dunia na Akhera, haitofautishi kati ya ukoo na ukoo, wala rangi na rangi, na watu wote ndani ya Uislamu ni sawa, hakuna mbora katika Uislamu kwa mwenzie isipokuwa kwa kadiri ya matendo yake mema.

Amesema Allah Mtukufu:

﴿مَنْ عَمِلَ صَٰلِحًا مِّن ذَكَرٍ أَوْ أُنثَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيَنَّهُۥ حَيَوٰةً طَيِّبَةً وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَجْرَهُم بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا۟ يَعْمَلُونَ ٩٧﴾

***"Mwenye kufanya tendo zuri, akiwa ni mwanamume au ni mwanake, na huku ni mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake , basi tutampa maisha mazuri (yenye utulivu duniani hata kama ni mchache wa mali), na tutawalipa huko Akhera thawabu zao kwa uzuri zaidi ya walivyofanya (duniani)".***

[An Nahli: 97].

Na miongoni mwa yale anayoyatilia mkazo Mwenyezi Mungu ndani ya Qur'ani tukufu nikuwa kumuamini Mwenyezi Mungu Mola Mlezi na muabudiwa, na Uislamu kuwa ndio dini, na Muhammadi kuwa Mtume ni jambo la lazima mwanadamu hana hiyari ndani yake; na siku ya Kiyama kuna hesabu na malipo; atakayekuwa muumini wa kweli basi atafuzu na kufaulu ufaulu mkubwa, na atakayekuwa kafiri basi atapata hasara ya wazi.

Amesema Allah Mtukufu:

﴿... وَمَن يُطِعِ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ يُدۡخِلۡهُ جَنَّٰتٖ تَجۡرِي مِن تَحۡتِهَا ٱلۡأَنۡهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَاۚ وَذَٰلِكَ ٱلۡفَوۡزُ ٱلۡعَظِيمُ ١٣ وَمَن يَعۡصِ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ وَيَتَعَدَّ حُدُودَهُۥ يُدۡخِلۡهُ نَارًا خَٰلِدٗا فِيهَا وَلَهُۥ عَذَابٞ مُّهِينٞ ١٤﴾

***"...na atakayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi atamuingiza katika pepo zipitazo chini yake mito, ataishi humo milele, na huko ndiko kufuzu kukubwa,***

***na atakayemuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake na akavuka mipaka yake, basi atamuingiza motoni, ataishi humo milele na atakuwa na adhabu yenye kudhalilisha".***

[Al-Nisaa: 13-14].

# Yaliyomo

Uislamu ....................................................................2

Ni dini ya maumbile na akili na furaha..................................2

Nani aliyekuumba? .............................................................2

Na je, inawezekana kuwa Mwenyezi Mungu alituumba kisha akatuacha hivhivi? Na je, inawezekana kuwa Mwenyezi Mungu aliumba viumbe vyote hivi pasina kuwa na lengo wala dhumuni yoyote?........................................................................6

Na kwakuwa tunajua fika kuwa sisi hatuwezi kuendesha maisha haya ya dunia pasina ya kila mtu kupata malipo ya yale aliyoyafanya kuanzia ya kheri au ya shari; kwa hivyo hapatokuwa na adhabu kwa madhalimu wala kuwalipa watenda wema?......7

❊❊❊

هدية
HADIYAH

## The Encyclopedia of Ar-Rahman's Guests

Selected material for Pilgrims and Um-rah teaching it in languages of the world.